

102/1

KISWAHILI INSHA

KARATASI YA KWANZA

SEPTEMBA 2022

MUDA: SAA 1 ¾

**MWONGOZO WA KUSAHIHISHIA**

**TATHMINI YA PAMOJA YA LANJET**

*Hati ya Kuhitimu Kisomo cha Sekondari Kenya (K.C.S.E)*

102/1

Insha ya Kiswahili

Karatasi ya 1

SAA 1 ¾

**MAAGIZO KWA MTAHINIWA:**

- 1) Mtahiniwa aandika jina lake, nambari ya mtihani na tarehe katika karatasi ya majibu.
- 2) Karatasi hii ina maswali manne.
- 3) Ajibu maswali ***mawili pekee***. Kila swali lina alama ishirini.
- 4) Swali la ***kwanza*** ni la ***lazima***.
- 5) Achague swali lingine ***lolote moja*** kutoka maswali matatu yaliyosalia.
- 6) Majibu yote yaandikwe kwa ***Kiswahili*** katika ***kijiabu cha majibu*** alichopewa.

*Matahini aoneshe alama za mwanafunzi sehehmu hii:*

SWALI	1	2	3	4	JUMLA
UPEO	20	20	20	20	40
ALAMA					

- 1. Ulisoma tangazo katika gazeti la Mzalendo kuhusu nafasi ya kazi ya udaktari. Baada ya kuandika ombi la kazi hiyo, umealikwa kwa mahojiano. Andika tawasifu- kazi yako utakayowasilisha.**

Mtahiniwa azingatie mambo yafuatayo:

- a) *Anwani* : *Iandikwe kwa herufi kubwa na ipigwe mstari. Aonyeshe ni tawasifu ya nani.*
  - b) *Utangulizi*: *mtahiniwa aoneshe usuli wake, tarehe ya kuzaliwa, wazazi n.k.*
  - c) *Mwili wa insha uonyeshe*:
    - *Maisha yake kuanzia utotoni*
    - *Maelezo ya kina kuhusu elimu yake*
    - *Ufanisi wake katika masomo- hasa unaolenga sayansi n.k*
    - *Mafanikio yake katika kazi mbali mbali alizofanya*
    - *Afafanue juu ya taaluma na tajriba yake*
    - *Aangazie pandashuka zake maishani*
    - *Aonyeshe uraibu wake na talanta (si lazima)*
- \*Maelezo yapangwe kiwakati kama yalivyofuatana
- d) *Awe na warejelewa*

**TANBIHI: Mtahiniwa aandika WASIFUKAZI**

*Akiandikwa kwa mtindo wa moja kwa moja atuzwe juu ya kumi.*

### ***Muundo wa Tawasifukazi***

*Wasifukazi huwa na anwani kuu yenye neno ‘WASIFUKAZI’ na vichwa vidogovidogo vyenye sehemu zifuataza*

### ***Maelezo ya binafsi***

- *Jina.*
- *Anwani.*
- *Umri.*
- *Uraia.*
- *Kitambulisho.*
- *Simu.*
- *Baruapepe.*

### ***Elimu***

- *Chuo kikuu.*
- *Chuo.*
- *Shule ya upili.*
- *Shule ya msingi.*

### ***Uzoefu wa kazi***

*Shirika/ kampuni na wakati wa kazi (anza na ile ya kwanza hadi ya sasa)*

### **Maelezo mengine kama;**

- *Uraibu.*
- *Shughuli katika jamii.*
- *Mchango katika ujenzi wa taifa.*
- *Shughuli nyinginezo.*

### **Warejelewa**

- *Cheo wanachoshikilia.*
- *Majina yao.*
- *Anwani zao.*
- *Simu na barua pepe.*
- *Wasizidi watatu ila wasipungue wawili.*

## **2. Serikali ni ya kulaumiwa kutokana na kuzorota kwa hali ya usalama nchini. Jadili.**

### **Kuunga**

- *Uchache wa maafisa wa usalama nchini.*
- *Ukosefu wa ajira nchini.*
- *Uchochole uliokithiri mionganoni mwa wanajamii.*
- *Kutotekeleza sera kuhusu mpango wa uzazi ambapo kuongezeka kwa idadi ya watu kunasababisha kung 'ang 'aniwa kwa rasilimali kama mashamba na nyinginezo.*
- *Kuwepo kwa silaha haramu mikononi mwa raia.*
- *Wachache kuruhusiwa kumiliki bunduki bila kufanyiwa uchunguzi wa sawa.*
- *Askari kuzembea kikazi au kukosa kutekeleza majukumu yao kama inavyotarajiwa.*
- *Kutokuwa na sera faafu kuhusu usalama wa mwanaainchi.*

### **Kupinga**

- *Serikali inafanya msako wa kitaifa kuwasaka na kuwatambua magaidid wanaojificha mionganoni mwa wananchi.*
- *Serikali ina mpango wa kuwasajili upya wananchi.*
- *Serikali imeanzisha mpango wa nyumba kumi.*
- *Ukiwa na fadhaa huwasukuma watu kufanya maovu.*
- *Kuwapo kwa misimamo mikali ya kidini ambayo baadhi yayo huhimiza mauaji.*
- *Vijana kukosa maelekezo faafu kutoka kwa wazazi.*
- *Kuvunjika kwa asasi za kijamii ambapo hapana uelekezi kwa wana.*
- *Jukumu la ulezi wa wana limeachiwa familia husika badala ya jamii nzima kama ilivyokuwa awali.*
- *Mazingira wanamokulia na kulelewa wanajamii (watoto wa mitaani)yanafunza uhalifu.*
- *Kutokuwa na msimamao sawa kuhusu suala zima la usalama mionganoni mwa viongozi.*

### **Tanbihi**

- ✓ Mtahiniwa anaweza kuwa na hoja nyingi za kuunga mkono na moja au zaidi za kupinga.
- ✓ Mtahiniwa anaweza kuwa na hoja nyingi za kupinga na moja au zaidi za kuunga.
- ✓ Mtahiniwa atoe msimamo wake.

- ✓ Katika hali zote mtahiniwa asiwe na chini ya hoja nane.
- ✓ Anayekosa kushughulikia pande zote mbili asipite alama 10.
- ✓ Mtahiniwa anaweza kutota hoja sawa pande zote alimradi atoe msimamo.
- ✓ Hakiki hoja zingine za mtahiniwa.

### **3. Andika kisa kitakachodhahirisha ukweli wa methali: Mjinga akierevuka, mwerevu huwa mashakani**

*Hii ni insha ya methali.*

*Kisa kidhahirisha mambo yafuatayo*

- *Mtu/ watu ambao wana tabia ya kuwadanganya wenzao au kuwatapeli watafikiwa na makuu pale wale wanaodanganywa wakierevuka na kuyatambua matendo yao*

**AU**

- *Viongozi wasiwafanyie maovu raia wawaongozao kwani wakiwatambua basi watakuwa mashakani kwani watavuliwa vyeo.*
- *Mtahiniwa abuni kisa ambacho waliokuwa na mazoea ya kuwadanganya wenzao wanafikia hali ambapo hila zao hugunduliwa na hivyo waathirirwa kuchukua hatua fulani dhidi yake au yao.*
- *Mtahiniwa aweze kuonyesha:*
  - Hali ya mwanzo ya mhusika kutapeli au kuhadaa wenzake*
  - Wahadaiwa kutambua hadaa au utapeli au udanganyifu kisha wanavyochukua hatua mwafaka kuhusu janmbo hilo*

#### **Tanbihi**

- Mtahiniwa akishughulikia upande momja pekee alama zisipite 10
- Anwani si lazima. Maana yamethali si lazima.

### **4. Andika Insha itakayoanza kwa maneno haya:**

*Baada ya kusafiri mwendo wa kilomita mbili hivi, watu wawili waliokuwa wamefunika nyuso zao kwa barakoa na bunduki mikononi...*

*Hii ni insha ya kiubunifu. Mtahiniwa abuni kisa ambacho chaangazia mamabo kama vile*

- *wizi*
- *ugaidi*
- *utegaji nyara*
- *uharamia n.k*
- *Mtahiniwa aonyeshe walichotendewa, walivyokabiliana na tukio hilo, walivyojinasua na hatima ya waathiri na waathiriwa.*
- *Mtahini ahakiki ukomavu wa lughya ya mtahiriwa na hoja alizotoa.*